JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

SHULE YA SEKONDARI MAKOGA,

S.L.P. 230,

NJOMBE.

14/12/2020.

KUMBU NA: ……..

Mwanafunzi…….

Kijiji cha …….

S. L. P. ……

NJOMBE.

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA MAKOGA WILAYA YA WANGING'OMBE MKOA WA NJOMBE MWAKA WA MASOMO 2021

Ninayo furaha kukuarifu kwamba, umechaguliwa kujiunga na elimu ya sekondari kwa kidato cha **KWANZA** katika Shule ya Sekondari Makoga iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe. Shule ipo umbali wa kilometa 30 Magharibi mwa mji wa Njombe.

Usafiri wa mabasi unapatikana kutokea Njombe mjini katika kituo cha mabasi. Nauli kamili ni shilingi 3000 toka Njombe mjini hadi shuleni.

Muhula wa masomo unaanza tarehe **11/01/2021** Na mwisho wa kuripoti shuleni ni IJUMAA ya tarehe **17/01/2021** tu.

Karibu sana Shule ya Sekondari Makoga.

E.T. MLOWE
MKUU WA SHULE

MAHITAJI YA MSINGI YA MWANAFUNZI SHULENI

SEHEMU YA KWANZA:

SARE MUHIMU ZA MWANAFUNZI SHULENI

a.) SARE ZA WAVULANA

i.) Suruali mbili rangi ya kijani jeshi kitambaa cha ISTIMU. Mshono-kawaida siyo modo.
ii.) Suruali mbili rangi ya Nyeusi kitambaa cha ISTIMU. Mshono wa kawaida na siyo modo.
iii.) Mashati mawili (02) meupe ya mikono mirefu.
iv.) Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili vya kamba (02) (siyo raba).
v.) Sweta mbili (02) mpya za rangi ya bluu.
vi.) Nguo za ndabi Bukta mbili (02)na chupi sita (06)
vii.) Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali (01).
viii.) Soksi jozi mbili (2) rangi nyeusi tu.
ix.) Jaketi jeusi kwa ajili ya baridi (**liishie kiunoni, lisiwe na kofia wala maandishi yoyot**e)

b.) SARE ZA WASICHANA

i.) Sketi mbili (02) rangi ya kijani jeshi, rinda box mbele na nyuma, ndefu ziguse kiatu kitambaa cha ISTIMU.
ii.) Magauni mawili (02) Rangi nyeusi, mshono wa solo, marefu, yaguse kiatu , yawe ya kitambaa cha ISTIMU.
iii.) Mashati mawili meupe mikono mirefu.
iv.) Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili vya kamba (02) (siyo bajaji au raba).
v.) Sweta mbili (02) mpya za rangi ya bluu.
vi.) Nguo za ndani: chupi sita (06) na taiti sita (06)
vii.) Kitenge kipya kizito doti moja (01)
viii.) Soksi nyeupe tu, jozi mbili (02) ziwe ndefu.
ix.) Jaketi jeusi kwa ajili ya baridi (**liishie kiunoni, lisiwe na kofia wala maandishi yoyot**e)
x.) Mahitaji mengine muhimu kwa ajili ya wasichana.

MUHIMU: WAISLAMU waje na hijabu hijabu nyeupe za darasani, nyeusi za nje ya darasa .

c.) SARE ZA MICHEZO KWA WOTE

i.) Viatu vipya vya michezo jozi moja (mfano: Raba)
ii.) Jezi mpya za michezo rangi ya njano au nyekundu .
iii.) Traki suti mpya rangi ya daki bluu jozi moja.
iv.) Tisheti mbili (02) za rangi ya kijivu

SEHEMU YA PILI:

MAHITAJI YA MWANAFUNZI DARASANI

i.) Begi jipya la kubebea daftari aendapo darasani .
ii.) Daftari kubwa kumi (10) aina ya kaunta.
iii.) Daftari ndogo kumi (10) za mazoezi ya darasani.
iv.) **Mafaili mawili (02) mapya (Spring file)** kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu.
v.) Mkebe mpya na vifaa vyake vyote.
vi.) Peni mpya 10 na penseli mpya 5
vii.) Rula mpya ya urefu wa sentimeta 30
viii.) **Bunda moja jipya** la karatasi za kufanyia mitihani kwa mwaka (RIMU) .

SEHEMU YA TATU:

MAHITAJI YA HOSTELI KWA MWANAFUNZI

a.) KWA AJILI YA USAFI

i.) Ndoo mpya yenye mfuniko ya lita kumi rangi **ya kijani na siyo rangi nyingine**
ii.) Ufagio mpya aina ya CHELEWA (KILA MWANAFUNZI).
iii.) Jembe jipya lenye mpini mpya (WASICHANA TU)
iv.) Kwanja jipya (WAVULANA TU).
v.) Sabuni za kufulia miche mitano
vi.) Mswaki mpya na dawa ya meno,
vii.) Mafuta ya kujipakaa
viii.) Kiwi na brashi,
ix.) Toilet pepa tano (5) za kuanzia.
x.) Kandambili mpya za kuogea

b.) KWA AJILI YA MATUMIZI BINAFSI BWENINI

i.) Tranka kubwa jipya moja lenye kufuli imara
ii.) Solata au tochi kwa ajili ya tahadhari ya usiku.
iii.) Godoro jipya futi tatu. (Godoro chapa ya Dodoma kwa ajili ya ubora).
iv.) Mashuka mawili (02) mapya ya rangi ya pinki.
v.) Blanketi mbili nzito mpya.
vi.) Mto wa kulalia mpya na foronya ya pinki.
vii.) Vyombo binafsi vya chakula: kontena, kikombe na kijiko.

SEHEMU NNE: MAHITAJI YA CHAKULA CHA MWANAFUNZI

i.) Mahindi: Debe kumi (10) kwa mwaka wa masomo
- Mwanafunzi atatoa debe (5) kila muhula

ii.) Maharage debe tatu (03) kwa mwaka wa masomo
- Debe moja na nusu (1½) kwa kila muhula.

KUMBUKA: Aina ya maharage yanayohitajika ni SALUNDE pekee.

iii.) Mchele debe moja(1) kwa mwaka sawa na kilo ishirini (20).
- kilo kumi (10) muhula wa kwanza na kilo (10) muhula wa pili

SEHEMU YA TANO: BIMA YA AFYA NA TAHADHARI

Mwanafunzi atatoa sh. 6,000 ya bima ya afya kwa agizo kwa sheria ya bima ya afya.

- Mwanafunzi mwenye bima ya afya ya NHIF hatatoa fedha hiyo shuleni.
- Fedha hii iletwe shuleni siku ya kufungua shule kwa mwalimu mlezi wa bweni.
  KUMBUKA: FEDHA YA BIMA ISILIPWE KUPITIA akaunti ya shule.

SEHEMU YA SITA: MALIPO YA FEDHA ZA UENDESHAJI WA HOSTELI

Kila mwanafunzi atalipa shilingi laki moja na elfu thelathini kwa mwaka (130,000/=) ya uendeshaji wa gharama za hosteli. Kila muhula atalipa shilingi elfu hamsini (65,000/=).

Kumbuka mambo manne unapolipia fedha hii uwapo benki au kwa mawakala wanaotambulika.

i.) Fedha ilipwe kupitia benki ya NMB au wakala wa NMB
ii.) Akaunti Namba ya shule **ni 60601000015**
iii.) Jina la akaunti ya shule ni **MAKOGA SEKONDARI** .
iv.) Kuandika Jina kamili la Mwanafunzi katika eneo la mlipaji kwenye risiti ya fedha. **MUHIMU SANA Usiandike jina la mzazi au mlezi. Jina la mlimpaji liwe la mwanafunzi mwenyewe**.

Fedha hii itatumika kama ifuatavyo:

i.) Kununulia kuni, vyombo vya jikoni na kusaga mahindi
ii.) Kununulia nyama, mafuta ya chakula, chumvi na sukari
iii.) Kununulia matunda na mbogamboga za majani
iv.) Kununulia vifaa vya usafi jikoni na mabwenini
v.) Kulipa posho kwa wapishi na msagishaji wa mashine
vi.) Kuendeshea gharama za matengenezo ya mashine.
vii.) Kusafirishia mizigo inayonunuliwa kama ilivyotajwa hapo juu.

FOMU YA KUJIUNGA NA ELIMU YA SEKONDARI MAKOGA

A: MAELEZO BINAFSI YAHUSUYO MWANAFUNZI

1. JINA LA MWANAFUNZI: _____
2. TAREHE YA KUZALIWA: _____
3. KIJIJI ALIPOZALIWA: _____WILAYA _____
4. MKOA WA: _____DINI:_____ DHEHEBU: _____

B: TAARIFA YA BABA NA MAMA MZAZI WA MWANAFUNZI

1. JINA LA BABA: _____JINA LA MAMA: _____
2. SIMU YA BABA: _____ SIMU YA MAMA _____
3. KAMILISHA TAARIFA ZA MAHALI ANAPOISHI MZAZI
   KIJIJI CHA: _____ KATA YA: _____
   WILAYA YA: _____ MKOA WA: _____ S. L. P. _____

C: TAARIFA YA MLEZI WA MWANAFUNZI

1. JINA KAMILI LA MLEZI :_____
2. MAHUSIANO: (Mjomba, shangazi, dada, kaka, bibi, babu binamu n.k.) _____
3. NAMBA ZA SIMU: _____ AU _____
4. KAMILISHA TAARIFA ZA MAHALI ANAPOISHI MLEZI
   KIJIJI: _____ KATA:_____WILAYA_____

D: TAARIFA YA AFISA MTENDAJI NA MWENYEKITI WA KIJIJI CHA MZAZI

1. JINA LA AFISA MTENDAJI WA KIJIJI:_____
2. KIJIJI CHA: _____ S.L.P. _____
3. SIMU YA AFISA MTENDAJI: _____ AU _____
4. JINA LA MWENYEKITI WA KIJIJI:_____
5. KIJIJI CHA: _____ S.L.P._____SIMU YA MWENYEKITI:_____

MUHIMU: Ikiwa mzazi au mlezi wa mwanafunzi anahama kijiji au anabadilisha anwani au namba ya simu, taarifa itolewe shuleni mapema.

Mimi mzazi au mlezi wa mwanzafunzi_____ nakiri kuwa taarifa zilizojazwa hapo juu ni sahihi na kweli tu.

SAHIHI YA MZAZI AU MLEZI: _____ TAREHE: _____

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA - REQUEST OF MEDICAL EXAMINATION

MAKOGA SECONDARY SCHOOL,

P.O. BOX. 230,

NJOMBE.

TAREHE:……..…….

PART A:

The Medical Officer,

…….....District/Regional/Referral Hospital,

P.O. BOX…….

……..

Please Examine Mr./Miss: _____ as to his or her physical and mental fitness for a full time schooling course. The examination should include the following categories (1-4) each category or sub category of which will render the applicant's ineligibility in case of any defect.

1.
   a.) Eye – sight ……..……..
   b.) Hearing ……
   c.) Limbs ……..
   d.) Speech …….
   e.) Venereal diseases…….
   f.) Leprosy ……..……..
   g.) Epilepsy ……..…….
2. Neuroses ……
3. Other serious diseases ……..…….
4. Pregnancy for girls ……...…….

Part B: MEDICAL CERTIFICATE (To Be Completed By A Medical Officer)

I have examined the fitness of the above candidate and consider that he / she is **physically / mentally fit/unfit** for a full time schooling course for further studies.

Date of examination:_____ Signature:_____

AHADI YA MWANAFUNZI

(IJAZWE NA KURUDISHWA KWA MKUU WA SHULE)

1. Mimi_____ nimesoma na kuelewa maelekezo, sheria, kanuni na taratibu za shule ya Sekondari Makoga. Nimekubali kuingia kidato cha _____ katika shule hii kuanzia tarehe _____
2. Kwa hiyo, naahidi kwamba:
   a.) Nitatii sheria zote za shule na kutimiza maagizo yote muhimu yaliyotajwa.
   b.) Sitashiriki katika vitendo vyoa HUJUMA wala vitendo ambavyo vitakuwa ni kinyume na sheria zote za shule na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
   c.) Nitatunza mali zote binafsi na shule kama majengo, samani, vitabu na kadhalika.
   d.) Sahihi ya Mwanafunzi:_____
   e.) Tarehe ya kusaini fomu:_____

KIAPO AU AHADI YAMZAZI AU MLEZI WA MWANAFUNZI

Mimi_____ ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi_____

NAAHIDI KWAMBA:

1. Nitashirikiana kikamilifu na uongozi, walimu na wafanyakazi wote wa Shule ya Sekondari Makoga katika kumsaidia, kumlea na kumwelimisha mtoto wangu. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa anazingatia sheria, taratibu na kanuni zote za shule na nchi ili aweze kutimiza maagizo yote yaliyotajwa hapo juu.
2. Nitafanya kila linalowezekana ili kumwezesha mwanangu kufika shuleni mapema. Nitamsaidia aweze kuishi mazingira mazuri ya kujifunzia. Nitamsaidia mahitaji yote muhimu ya shule kwa wakati wote akiwa shuleni.
3. Nitaitika wito wa mkuu wa shule na walimu ili niweze kusaidiana nao katika makuzi na malezi ya mwanangu ili afikie ndoto ya maisha yake kupitia Shule ya Sekondari Makoga.

SAHIHIYA MZAZI / MLEZI: _____ TAREHE:_____

SHULE YA SEKONDARI MAKOGA

SHERIA ZA SHULE

1. Mwanafunzi anatakiwa kusimama kumsalimia mtu yeyote anayemzidi umri wakati wote na mahali popote.
2. Mwnafunzi anatakiwa kuheshimiana nakushirikiana na wenzake.
3. Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu na kufanyakazia anazopewa.
4. Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu bendera ya taifa, wimbo wa taifa, fedha ya taifa wakati wote.
5. Mwanafunzi anatakiwa kuwa msafi na kutunza mazingira vizuri.
6. Mwanafunzi awapo shuleni lazima alale katika bweni husika pekee.
7. Mwanafunzi anatakiwaa kuwa mfano mwema ndani na nje ya shule.
8. Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu ofisi ya mkuu wa shule, ofisi zote za shule, ukmbi wa chakula, maktaba na madarasa.
9. Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria masomo yote kwa wakati na kufanya mitihani inayomhusu.
10. Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria mikutano yote shuleni kama vile; kupandisha bendera ya taifa, baraza la shule, mikutano ya bweni, darasa nk.
11. Mwanafunzi anatakiwa kutii kengele kama mwito wa haraka.
12. Mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare rasmi ya shule kama ifuatavyo:
    - Darasani
    - Anapotoka nje ya shule
    - Anaporejea shuleni
    - Wakati wa baraza la shule
13. Mwanafunzi atatoka nje ya shule kwa ruhusa maalum ya:
    - Mwalimu wa zamu na kuwepo tena shuleni kabla ya saa 12:00 jioni.
    - Mkuu wa shule tu kwa kibali maalum cha kulala nje ya shule.

      NB: mwanafunzi akilala nje ya shule bila ruhusa atakuwa amejifukuza shule mwenyewe.
14. Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea nyumba za walimu na watumishi wengine ila kwa kibali maalum tu. NB: Maeneo haya ni sawa na kuwa nje ya mipaka ya shule.
15. Mwanafunzi haruhusiwi kuingiza mgeni yeyote bwenini au darasani.
16. Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea au kujihusisha na maeneo yafuatayo:
    - Vilabu ya pombe (Bar).
    - Majumba ya kufikia wageni. (Guest houses).
17. Mwanafunzi anatakiwa kutunza mali zote binafsi pamoja na mali za umma kama vile madawati, vitanda, vifaa ya chakula, vitabu na vifaa vya maabara pamoja na majengo yote ya shule.
18. Mwanafunzi haruhusiwi kwa namna yoyote kumiliki au kutumia vifaa vinavyotumia umeme awapo shuleni kama vile: SIMU, JIKO, HEATER, RADIO nk.

MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

1. Wizi.
2. Uasherati, ubakaji na ushoga.
3. Uvutaji wa bangi na madawa ya kulevya.
4. Kumtukana, kumpiga mwalimu au mtumishi wa shule.
5. Kuoa au kuolewa.
6. Mimba, kutoa mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
7. Kutoa lugha chafua au matusi.
8. Kupatikana na makosa ya jinai.
9. Kugoma, kuchochea au kuongoza migomo shulenii.
10. Kukataa adhabu halali kwa makusudi.
11. Kumiliki au kupatikana na simu au vifaa vya simu.

UJAZAJI WA FOMU

Kabla ya kufika shule ya sekondari Makoga jaza fomu zifuatazo kwa umakini.

a.) Fomu ya taarifa binafsi za mwanafunzi uliyopewa.
b.) Fomu ya kupima afya. (Medical examination form). Hakikisha fomu hii inajazwa katika hospitali ya serikali ya wilaya. Kumbuka: Usiijaze fomu hii katika vituo vya afya au zahanati.

TAARIFA MUHIMU KWA WAZAZI WOTE

1. Mwanafunzi wa kidato cha kwanza aripoti shuleni siku ya JUMATATU ya tarehe 11/01/2021 saa moja kamili asubuhi akiwa na mzazi au mlezi wake kwa ajili ya usajili.
2. Mzazai afike na cheti cha kuzaliwa cha mwanafunzi siku JUMATATU ya TAREHE 11/01/2021 kwa ajili ya usajili wa mwanae.
3. Kikao cha wazazi wote kitafanyika siku ya ALHAMISI ya tarehe **14/01/2021** Muda kufika ni saa mbili kamili asubuhi.
4. Mzazi aje na risiti kamili ya malipo benki ya sh.65,000 za hosteli siku ya kikao.
5. Michango mingine ya chakula (CHAKULA NA FEDHA YA BIMA YA AFYA) itapokelewa siku ya JUMATATU ya tarehe 11/01/2021 tu, ambayo ndiyo siku ya kuripoti kidato cha kwanza.

…….

E.T. MLOWE

MKUU WA SHULE

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

FOMU YA MWANAFUNZI ANAYEHAMIA SHULE YA SEKONDARI MAKOGA

A: MAELEZO BINAFSI YAHUSUYO MWANAFUNZI

1. JINA LA MWANAFUNZI: _____
2. TAREHE YA KUZALIWA: _____
3. KATA ALIPOZALIWA MWANAFUNZI: _____
4. WILAYA _____MKOA WA: _____
5. DINI:_____ DHEHEBU: _____

B: TAARIFA YA BABA/MAMA MZAZI AU MLEZI WA MWANAFUNZI

1. JINA LA BABA MZAZI WA MWANAFUNZI: _____
2. JINA LA MAMA MZAZI WA MWANAFUNZI: _____
3. JINA LA MLEZI WA MWANAFUNZI: _____
4. NAMBA ZA SIMU: _____ AU _____

C: TAARIFA ZA MAHALI ANAPOISHI MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI

KATA: _____WILAYA _____ MKOA _____ S. L. P. _____

D: TAARIFA ZA SHULE ALIYOHAMA MWANAFUNZI

1. JINA LA SHULE ULIYOHAMA: _____
2. ANWANI YA SHULE ULIHAMA:_____
3. KATA ULIYOHAMA: _____
4. WILAYA ULIHAMA (KAMA NI NJE YA WANGING'OMBE): _____
5. MKOA ULIOHAMA (KAMA NI NJE YA NJOMBE):

   _____

Mimi mzazi au mlezi wa mwanafunzi_____nakiri kuwa taarifa zilizojazwa hapo juu ni sahihi na kweli tu.

SAHIHI YA MZAZI AU MLEZI: _____ TAREHE: _____